# YOTE UNAYOHITAJI KUJUA KUHUSU

# MCHOCHOTA WA INI WA C

## Mchochota wa Ini wa C ni nini?

Mchochota wa Ini wa C yani Hepatitis C (HCV) ni virusi vinavyoshambulia ini. Ini hufanya kazi kama kichujio cha mwili kwa kuondoa sumu (vitu vyenye madhara) kutoka kwa chochote unachokula, kunywa, kuvuta, kuingiza kwa sindano, au kuingiza kwenye mwili wako.

## Je, ulijua?

Ini ni muhimu kwa afya yako. Ini husaidia katika kumeng'enya chakula na kuganda kwa damu



Huwezi kuishi bila ini yako!

## Dalili za Mchochota wa ini wa C



Njano ya macho na ngozi (Jaundice)



Maumivu ya tumbo



Kichefuchefu au kutapika



Uchovu mwingi



Homa



Kupoteza hamu ya kula



Mkojo wa rangi ya kahawia na kinyesi chepesi au Kuhara

## Ugonjwa wa Mchochota wa Ini wa C

- Unadumu miezi 6 au chini
- Asilimia 15-25 ya watu watapata dalili
- Mwili wako unaweza kutoa virusi peke yake bila matibabu
- Hata kama umepata virusi kutoka kwa mwili wako au kupitia matibabu, bado unaweza kupata HCV tena

VS

## Mchochota wa Ini ya C ya Mfululizo

- Magonjwa ya maisha yote ikiwa haijatibiwa
- Zaidi ya 50% ya watu wazima walio na HCV ya papo hapo wataendelea kuwa na HCV ya mfululizo
- Ikiwa haijatibiwa, matatizo makubwa kama vile cirrhosis (kuweka makovu kwenye ini), kansa ya ini, na hata kifo vinaweza kutokea
- Matibabu yanaweza kukupa uponyaji na kuzuia matatizo makubwa

## Kuelewa Matokeo ya Vipimo

### Kingamwili (Uchunguzi)

- Kipimo hiki kinabaini ikiwa umewahi kuathiriwa na virusi vya Mchochota wa Ini wa C.
- Mara tu unapogundulika kuwa na mchochota wa ini wa C, kipimo chako cha antibodi kitabaki chenye majibu chanya (positif) kwa maisha yako yote, hata kama utatibiwa na kuponywa.

### Aina za Vipimo

Kuchomwa kidole au Kuchukua damu





### RNA (Kuthibitisha)

- Kipimo hiki kinabaini ikiwa kwa sasa una virusi vya Mchochota wa Ini wa C mwilini mwako.
- Ikiwa imegunduliwa (chanya), basi una virusi vya Mchochota wa Ini wa C kwenye mwili wako na unaweza kuambukiza wengine kwa virusi hivyo.
- Ikiwa hakugundulika (negativi), basi huna virusi vya hepatitis C mwilini mwako na huwezi kuambukiza wengine.

### Aina za Vipimo

Kuchukuwa damu



YOTE UNAYOHITAJI KUJUA KUHUSU

# Kujilinda Mchochota wa Ini wa C



## Mchochota wa Ini wa C inasambaje

1. Mchochota wa Ini wa C huambukiza wakati damu ya mtu aliye na Mchochota wa Ini wa C inachanganyika na kiasi kidogo cha damu, kisichoonekana, cha mtu asiye na Mchochota wa Ini wa C.
2. Mchochota wa Ini wa C pia inaweza kupitishwa wakati wa ujauzito na kujifungua ikiwa mjamzito ana Mchochota wa Ini wa C ambayo haijatibiwa.

**Mchochota wa Ini wa C pia inaweza kuambukizwa kupitia vitendo vya kuchomelea na kupigia tatoo visivyo safi. Daima nenda katika kituo kilichosajiliwa.**



## MATIBABU

- Uharibifu wa ini unaweza kutokea katika kipindi cha miezi hadi miaka, hivyo kuanza kutibu mapema ni bora.
- Matibabu ya Mchochota wa Ini wa C yanaweza kuwa rahisi kama kuchukua vidonge 1-3 kwa siku kwa muda wa miezi 2-3.
- Watu wengi hugalimia madhara machache au hakuna madhara kabisa kutoka kwa dawa za matibabu.
- Zaidi ya 95% ya watu waliotibiwa wanapona.

### Je, Kuponywa Kunamaanisha Nini?

- Virusi vya Mchochota wa Ini wa C havipo tena kwenye damu yako.
- Hauwezi tena kuambukiza kwa wengine.
- Unaweza kupata Mchochota wa Ini wa C tena ikiwa utagusa damu iliyoambukizwa, kwa hivyo jilinde kugusu damu ya mtu mwingine yeyote.

## KUMBUKA

- Hudhuria miadi yako yote, ikiwa ni pamoja na ile baada ya kumaliza matibabu.
- Tumia dawa kama ilivyoagizwa na kufuata maagizo ya mtoa huduma ya afya.

## USI SHIRIKISHE....

vitu vya kibinafsi ambavyo vinaweza kuchafuliwa na damu



Vifaa vya Kutibu Kisukari | vitu vya kukata kucha | Mswaki wa meno | Wembe

Vifaa vya sindano au kuvuta



Dawa au dawa za kuingizwa kwa sindano | Dawa ya kufukizia pua au mifereji ya kuvuta pua

## Jinsi Ya Kulinda Wapendwa Wako




Funika majeraha | Tumia kondomu wakati wa kujamiiana | Safisha uso kwa kutumia suluhisho la dawa ya kunasa (bleach)

## Pimwa, Matibabu Yanaponya!

Vituo vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa (Centers for Disease Control (CDC)) wanapendekeza kuwa watu wazima wote wapimwe kwa Mchochota wa Ini wa C angalau mara moja kwa maisha yao.
Piga simu kwa idara ya afya ya eneo lako ili kupanga kipimo chako leo!

Piga scan au bonyeza kutafuta idara ya afya karibu nawe!

ZUNGUMZA. PIMA. TIBU.

Dept. of Health, Authorization # MT7UY9-1, electronic only, March 31, 2025. This public document was promulgated at a cost of $Electronic per copy.